# MUMIAS / BUNGOMA JOINT SCHOOLS

# MUHULA WA KWANZA - 2020

# DARASA LA NANE

# <u>KISWAHILI:</u>

# LUGHA

MUDA : Saa 1 Dakika 40

***<u>SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO</u>***

1. Umepewa karatasi hii ya maswali na karatsi ya kujibu. Karatasi hii ina maswali 50
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika karatasi hii
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika KARATASI YA MAJIBU na wala siyo katika karatasi hii ya maswali.

***JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU***

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo umeyaandika katika karatasi ya majibu.

**NAMBARI YAKO YA MTIHANI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye nambari zinazokuhusu, onyesha nambari yako kamili ya mtihani ( yaani nambari ya shule, na zile nambari tatu za mtihani ) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
9. Kwa kila swali 1—50, umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A,B,C,D. Ni herufi uliyochagua kuwa ndiyo jibu.

**Kwa mfano:**
Chagua jibu sahihi kwa swali 16.

16. Ni sentensi ipi iliyotumia kirejelei kwa usahihi ?

A. Miti iliokatwa ni mirefu. B. Mikunga iliyovuliwa ni minono
C. Minyoo iliyokufa imeondolewa D. Anakoishi ni safi

Jibu sahihi ni **D**
Katika karatasi ya majibu:
15. (A) (B) (C) (D) 16. (A) (B) (C ) ~~(D)~~ 17. (A) (B) (C ) (D)

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali nambari 20, kisanduku chenye herufi D ndicho kilisho chorwa kistari.

10. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku. ulivyopewa

**Karatasi hii ina maswali 50 iliyopigwa chapa.**

**FUNGUA UKURASA**

***Imepigwa chapa na H. S. Said Printers—Bungoma***
***Rununu : 0720-714044 / 0712-137046***

**Soma vifungu vifuatavyo vina nafasi 1-15 kisha chagua jibu lililo sahihi kujazia nafasi zilizoachwa wazi.**

Nchi hii-1- na nzige ambao wamehamia maeneo mengi nchini -2- inastahili kufikiria kwa makini mbinu ambazo -3- matunda katika juhudi hizo. Nzige wameendelea kuvamia sehemu mbalimbali nchini na -4- hofu kuu ya kushuhudiwa kwa baa -5- njaa nchini, -6- ikiwa hazitaweza -7-.Lakini hali iliyo na mambo -8- kushuhudiwa katika -9- cha mwezi mmoja uliopita ni wazi kwamba serikali imeshindwa kuwakabili wadudu hao.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. A. kukabili | B. kukabiliana | C. kukabiliwa | D. kukabilia |
| 2. A. ; | B. , | C. : | D. . |
| 3. A. zitazalisha | B. zitazaana | C. zitazaa | D. zitazalia |
| 4. A. kazibua | B. kuziba | C. kuchubua | D. kuibua |
| 5. A. ya | B. la | C. za | D. cha |
| 6. A. huenda | B. yakini | C. hasa | D. pindi |
| 7. A. kudhibitiwa | B. kuthibitisha | C. kuthibitiwa | D. kudhibitisha |
| 8. A. inayoendelea | B. zinazoendelea | C. vinavyoendelea | D. yanayoendelea |
| 9. Kipindi | B. muda | C. wakati | D. saa |

Visanga vya Bezo vilishamiri siku-10- siku. Wazazi wake walizongwa na hofu kuhusu kitinda mimba -11- kutomaliza kazi za ziada shuleni -12-. Walimu wake wakalazimika kumeza mrututu kutokana na mchezo wake wa kawaida. Matusi kwa wenzake -13- kipaumbele nayo adhabu ya walimu ikawa -14-. Muhula wa tatu ulipomlemea akaamua kugura kwenda mjini kutafuta kazi kwa -15- wa mlanguzi mmoja mjini, Bwana kamaliza.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 10. A. baada ya | B. kabla ya | C. badala ya | D. zaidi ya |
| 11. A. wao | B. yao | C. waje | D. yake |
| 12. A. kukawasheria | B.kukawa mwata | C. kukawa mwiko | D. kukawa ibada |
| 13. A. akaipa | B. akayapa | C. akaupa | D. akalipa |
| 14. A. dhahiri shahiri | B. balaa belua | C. kinu na mchi | D. bure bilashi |
| 15. A. mwamko | B. makaribisho | C. mwaliko | D. maagano |

**Kutoka swali 16 mpaka 30 chagua jibu lililo sahihi kulingana na maelezo uliyopewa**

16. Maneno yafuatayo yanafuatana vipi katika kamusi
    (i) Dharau
    (ii) Dhabihu
    (iii) Dhamana
    (iv) Dhambi

    A. (ii), (iv), (iii), (i) B. (i), (iii), (iv), (ii)
    C. (ii), (iii), (iv), (i) D. (i), (iv), (iii), (ii)

17. Umoja wa " seremala aliharibu ua wa nyumba yake"
    A. Maseremala waliharibu nyua za nyumba zao
    B. Maseremala waliharibu maua ya nyumba zao
    C. Seremala aliharibu nyua za nyumba zao
    D. Seremala waliharibu maua ya nyumba zao

18. Chagua jibu lenye nomino katika ngeli ya YA-YA
    A. Madini, mazao
    B. Magugu, makogo
    C. Mada, mahari
    D. Mazingira , mazingara

19. Chagua jibu lenye maelezo sahihi
    A. Kisugudi ni sehemu ya nyuma ya kichwa
    B. Bega ni kiungo cha mkono kati ya kiwiko na kisugudi
    C. Utosi ni sehemu ya juu na nyuma ya kichwa
    D. Kitanga ni sehemu ya mwisho ya mkono yenye vidole

20. Chagua kinyume cha ' Wenyeji waliondoka baada ya eropleni kutua'
   A. Wenyeji waliondoka kabka ya eropleni kutua
   B. Wageni waliwasili kabla ya eropleni kupaa
   C. Wageni waliondoka kabla ya eropleni kutua
   D. Wageni waliondoka baada ya eropleni kutua

21. Chupio, kikuba kilinzi ni mapambo kama vile kashida, jezi, deraya ni _______
   A. michezo  B. Mavazi
   C. zana za vita  D. ala

22. Akisami $^{7}/_{10}$ kwa maneno ni
   A. Ushuru saba  B. Ushuri saba
   C. Subui kumi  D. Thumni saba

23. Chagua sentensi iliyo katika kauli ya Kutendeka.
   A. Juma aliandika barua kwa makini
   B. Nguo alizozianika zilikauka upesi
   C. Chakula hiki hakipikiki kutokana na maandalizi mabovu.
   D. Tuliamka mjini siku ya Alhamisi

24. Ni maelezo yapi ambayo si sahihi?
   A. Kituo ni mshororo wa mwisho wa kila ubeti
   B. Thenini ni shairi lenye mishororo minane katika kila ubeti
   C. Ukingo ni kipande cha nne cha mshororo
   D. Mleo ni mshororo wa pili katika ubeti

25. Onyesha sentensi yenye kielezi cha mahali
   A. Tulisimama ukingoni
   B. Mtihani utaanza mwakani
   C. Wanafunzi walicheza alasiri
   D. Tulimeza tembe mara tatu

26. Kiambishi 'kwa' katika sentensi " Alichanja kuni kwa shoka" kimetumikaje?
   A. Kuonyesha kusudi
   B. Kuonyesha uhusiano
   C. Kuonyesha ala ya matumizi
   D. Kuonyesha ulinganisho

27. Unda nomino kutokana na kitenzi 'Shajiisha'
   A. Shajiishiwa  B. Shujaa
   C. Kushajishia  D. Shajiishia

28. Tambua aina ya maneno katika sentensi ifuatayo: Madarasa yote yalikuwa na wanafunzi kadhaa
   A. Nomino, kivumishi, kitenzi, kiunganishi, nomino, kivumishi.
   B. Nomino, kiwakilishi, kitenzi, kiunganishi, nomino, kivumishi
   C. Nomino, kivumishi, kitenzi, kiunganishi, nomino, kiwakilishi.
   D. Nomino,kivumishi, kitenzi, kiunganishi, nomino, kielezi

29. Chagua tamathali za lugha zilizotumika katika sentensi hii.
   "Chudi anafanya kazi mithili ya mchwa"
   A. Nahau, tashbihi
   B. Chuku, sitiari
   C. Tabaini, sitiari
   D. Majazi, tashbihi

30. Upande wa dira kati ya kaskazini na kaskazini mashariki ni?
   A. Kaskazini mashariki
   B. Kaskazini ya mashariki kaskazini
   C. Kaskazini ya kaskazini mashariki
   D. Mashariki ya kaskazini kaskazini

**<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31-40.</u>**

Biashara ya matatu nchini Kenya ina historia ndefu na yenye mabadiliko chungu nzima. Je, unajua asili ya neno matatu? Magari haya mwanzoni yaliwasafirisha abiria mijini na kulipisha mapeni matatu safari yoyote ile. Kwa muda mrefu nauli ilikuwa ni hiyo hiyo wakati wowote mwendo wowote kwa sababu hii yakaja kujulikana kama matatu. Jina hili lilikubalika mingoni mwa wakenya wa jamii zote na hutambulika katika lugha zote nchini. Linalokubalika pia katika lugha ya Kiswahili.

Kwa muda mrefu, magari ya matatu yalifanya biashara bila kuzingatia nidhamu barabarani. Wenye matatu na madereva walikuwa hawasikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini. Walipakia abiria magarini kama bidhaa na kubeba zaidi ya kiasi kilichotakikana. Waliendesha magari yao kwa kasi kama umeme huku wakishindania abiria. Utingo au manamba waliwashawishi abiria kuingia katika magari yao na hata kuwavuta au kutwaa mizigo

yao wakielekeza kwenye matatu bila idhini ya msafiri. Daima wasafiri walikuwa katika tishio la kuibiwa mali yao katika vituo vya magari.

Baadhi ya wenye matatu waliendesha magari mabovu na yasiyofaa barabarani. Askari wa trafiki nao walikuwa hawajali bora tu wapokee kile walichokiita <u>'kitu kidogo'</u> waliruhusu magari yaliyovunja sheria kubeba abiria.

Matokeo ya mambo hayo yalikuwa ajali nyingi barabarani. Maelfu ya watu waliyapoteza maisha yao na wengine wengi kujeruhiwa na kulemazwa katika ajali za magari. Kwa kweli ulikuwa ni usiku wa giza nene.

Hauchi hauchi kunakucha na hakuna marefu yasiyokuwa na mwisho. Mwanzoni mwa mwaka wa elfu mbili na nne hali hii ilibadilika kabisa. <u>Uliokuwa usiku wa giza ukawa mchana wenye nuru na matumaini makubwa.</u>

Serikali kupitia kwa wizara ya uchukuzi na mawasiliano ilitangaza kuwa lazima magari haya yazingatie sheria zote za usafiri. Aidha lazima kila matatu iwe na kidhibiti mwendo ili kupunguza ajali zinazotokana na mwendo wa kasi.

Magari haya yalitakiwa yawe pia na mikanda ya usalama na kila abiria kondakta na dereva lazima ajifunge. Jambo hili lingesaidia kuzuia matatu kubeba watu wengi kuliko inavyofaa na vilevile kuzuia abiria kuumia sana wakati wa ajali.

Kila matau ilitakiwa kuandika wazi wazi pembeni idadi ya abiria inayofaa kubeba na sehemu inazofika.

Madereva na makondakta nao walitakiwa wavae sare ili watambulike kwa urahisi. Vilevile walilazimika kuwa na vitambulisho vya kazi. Dereva alitakiwa aweke picha yake mahali wazi garini ili abiria waweze kudhibitisha kuwa wanabebwa na dereva afaaye.

Kuna leseni tofautitofauti na stakabadhi nyingine ambazo kila matatu lazima iwe nazo kabla ya kubeba abiria. Hizi ni kama vile leseni ya barabarani, leseni ya bima, leseni ya dereva na barua nyinginezo.

Askari wa trafiki nao walitakiwa kukoma kupokea hongo. Waliopatikana wakipokea hongo walichukuliwa hatua kali na hata kupigwa kalamu. Vyombo vya mawasiliano kama vile runinga na magazeti vilichangia kutimiza haya kwa kuzingatia askari wa trafiki walionaswa na kamera walipopokea rushwa.

Kwa vile serikali ilikuwa imara katika msimamo wake, sheria hizo zote zilianza kuzingatiwa. Matatu zilikoma kubeba abiria ovyovyo, zikawa na vidhibiti mwendo, mishipi ya usalama na nidhamu ikawapo katika sekta hii. Abiria sasa hufurahia safari zao na huwa hawana hofu wanapokuwa safarini kwa kuwa ajali za barabarani zimepungua kabisa. Zamani abiria walisafiri roho mkononi, lakini leo huwa wamestarehe. Si ajabu wengine hujipumzisha kwa kulala garini na hivyo kufika waendako wakiwa si wachovu.

31. Kulingana na aya ya kwanza
   A. Biashara ya matatu nchini ni ya historia
   B. Biashara ya matatu imeshuhudia mabadiliko anuwai
   C. Jina matatu ilitokana na lugha ya Kiswahili na lugha nyingine nchini.
   D. Magari yaliwasafirisha abiria mara tatu kwa safari yeyote ile

32. Kulingana na ufahamu kutozingatia sheria
   A. Kuliwafanya maderva kutosikia la mwadhini wala la mteka maji msikitini
   B. Kuchangia wenye matatu kufanya biashara kwa muda mrefu
   C. Kulizidisha ajali nyingi barabarani
   D. Kusababisha watu kulala garini na kutumia vidhibiti mwendo

33. Kulingana na aya ya pili si kweli kusemma kuwa ___
   A. Abiria waliingia garini kwa kushurutishwa
   B. Wizi ulishuhudiwa katika vituo vya magari
   C. Wenye matatu na madereva walikaidi sheria za usafiri

D. Abiria waliabiri garini kwa hiari licha ya kuvutwa na mizigo yao kutwalliwa

34. Kwa mujibu wa taarifa, ' kitu kidogo ina maana;
   A. Nauli isiyoafiki
   B. Malipo ya trafiki
   C. Faini kwa polisi
   D. Zunguka mbuyu

35. Ni jibu lipi si hasara ya kutozingatia sheria za barabara
   A. Ulemavu
   B. Mauti
   C. Ajali nyingi
   D. Usiku wa giza nene

36. Mabadiliko katika sekta ya uchukuzi yalianza mwaka upi?
   A. 2003  B. 204
   C. 2004  D. 2008

37. Mikanda ya usalama
   A. ilizuia abiria kuumia zaidi
   B. Ilipunguza idadi ya abiria garini
   C. ilitumika zaidi na utingo na dereva
   D. Ilizuia ajali nyingi za barabarani

38. " Ulikuwa usiku wa giza ukawa mchana wenye nuru na matumaini makubwa" ina maana:
   A. Usiku ulitoweka na kuukaribisha mwangaza
   B. Wahudumu wa magari walilazimika kutii sheria na ajali kupungua
   C. Wizara ya uchukuzi na mawasiliano ilitangaza kuzingatiwa kwa sheria.
   D. Kila gari lilikuwa na kidhibiti mwendo

39. Kulingana na kifungu
   A. Ni rahisi kuwatambua utingo na madereva kutokana na maandishi pembeni mwa gari
   B. Matatu ya hapo awali yalikosa leseni muhimu, swala lililovuruga sekta ya uchukuzi
   C. Waliowahonga maafisa wa trafiki walichukuliwa hatua kali za kisheria
   D. Vyombo vya mawasiliano vilipunguza idadi ya wapokeaji rushwa

40. Kulingana na aya ya mwisho
   A. Sheria zilianza kuzingatiwa kabla ya serikali kutoa msimamo wake
   B. Baadhi ya abiria wangali wanasafiri kwa hofu tele
   C. Mabadiliko katika kusafiri bila tatizo lolote
   D. Uchovu wa usafiri huadhiriwa na aina ya matatu.

**<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41-50.</u>**

Kazi ni sehemu muhimu sana katika maisha ya mtu aliye na afya. Aliyesema ajizi ni nyumba ya njaa aligonga ndipo. Ni hali ya kukera na kukereketa maini umwonapo mtu aliye na afya akilaza damu. Mambo yalikuwa tofauti katika maisha ya kisogoni. Wazee wetu walitarajia kufanya kazi. Wale ambao walijikalia bila kujihusisha na kazi yoyote walisutwa kupitia kwa nyimbo, vitendawili, hadithi pamoja na methali. Ikumbukwe kuwa nyakati hizo, kazi aliyoifanya mtu ilitegemea umri, jinsia na nafasi ya mtu katika jamii husika. Wale ambao waliruhusiwa kutofanya kazi ni waliokuwa dhaifu, wagonjwa na wazee ambao hawakuwa na udole wa kufanya kazi. La msingi ni kuwa mwanajamii alistahili kufanya kazi na si kufanya tu bali kwa bidii na kujitolea.

Mambo sasa ni kinyume. Pana dhana kuwa wale waliosoma na kuhitimu masomo ya chuo kikuu hawana kazi. Fikra hii ni finyu ikiwa si potovu. Mtu humaanisha nini na anayelengwa ni nani? Ni jambo la kusikitisha au kuumiza matumbo kushikilia kuwa ikiwa mtu hajaajiriwa basi hana kazi. Msimamo huu ni hasi, mbovu na kuyakosesha maisha maana. Wapo watu wengi ambao wanaendelea kulisukuma gurudumu la maisha kwa kujihusisha na amali zao walizojipa wao wenyewe. Watu hawa wamedhihirisha bayana kuwa kujiajiri kuna faida za kipekee.

Ushaidi upo kuonyesha kuwa watu waliofaulu sana maishani ni wale wanaojihusisha na kazi zao. Wao hujiratibu shughuli zao za kila siku huwa na uhuru wa kuamua watafanya hiki ama kile . Mtu huyu huwa na uamuzi kuhusu ni jambo lipi la kumpa faida na lipi linaweza kumletea hasara. Ana uhuru wa kuacha amali hasi na kushughulikia zile chanya. Vile vile mtu

huyu ana uamuzi wa mwisho ikiwa ataendelea kufanya kazi hiyo au kuiandama nyingine ambayo pato lake ni bora zaidi.

Serikal ina jukumu na wajibu wa kutangaza shughuli zake ili kusaidia kupunguza uhamiaji wa watu mjini kwa kusingizia kutafuta kazi, ikiwa miundo msingi itatengenezwa mashambani na mirundikano hii ya watu majijini. Isitoshe maisha ya watu wa mashambani yatainuliwa. Bila shaka, utajiri wa taifa utakuwa umesambazwa kote nchini.

Mwelekeo wa watu kuhusu kazi za mikono sharti ubadilike. Pana imani mbovu kuwa wale ambao wanafanya kazi za mikono hawajasoma. Watu wengi huwapuuza na kuwatweza wanaozifanya kazi hizi. Wao huwa hawajaheshimiwa na hata utajiri wao huwa duni. Ni lazima kama ibada kuubadilisha msimamo huu. Tuanze kuziheshimu kazi hizi na kujenga mwelekeo chanya kuzihusu na kuhusu wanaozifanya. Ni vyema sisi sote tutambue kuwa sote hatuwezi kuwa matabibu au wahandisi. Ikiwa hali itakuwa hivyo, basi ni nani atawafundisha watoto wa wenzake? ni nani atampikia mwenzake na ni nani atakayemlimia mwenzake shamba? Kwa hivyo jinsi vidole vya mikono hupitishana kwa urefu, ndivyo mambo yalivyo kuhusu kazi zifanywazo na watu. Zote ni tofauti. Katika kutofautiana huko ndipo sisi hupata ujumi na urembo wa maisha. Kwani dunia ingekuwa vipi ikiwa rangi ni moja tu, samawati?

41. Ni jambo lipi ambalo linamkasirisha mwandishi?
   A. Watu wasiolaza damu
   B. Watu wanaokataa kazi
   C. Watu wanaotarajia kufanya kazi
   D. Watu walio na afya kukataa kazi

42. Ni sahihi kusema kuwa hapo awali
   A. Kazi ilitengwa kwa msingi wa kijinsia
   B. Kazi ilikuwa na wa kuifanya
   C. Kazi ilifanywa na wachache
   D. Kazi haikuheshimiwa

43. Kulingana na aya ya pili kinachomkera mwandishi ni watu
   A. Kudai hawana kazi
   B. Kudai wana kazi licha ya kutosoma
   C. Kusema hawana kazi licha ya kuhitimu umri wa kupata kazi
   D. Kudai kuwa wananyimwa kazi

44. Ni sahihi kusema kuwa
   A. Wapo wachache wanaohangaika
   B. Wapo wengi ambao hawatajiajiri
   C. Wapo watu ambao wamejiajiri
   D. Wapo wengi wanaoumizwa na ajira

45. Kwa mujibu wa kifungu; Umuhimu wa kujiajiri si
   A. Kujiamulia kazi ya kufanya
   B. Kujiamulia wakati wa kufanya kazi husika
   C. Kujiamulia hasara ya kupata
   D. Kujiamulia mkondo wa maisha

46. Serikali itahakikisha vipi watu wengi hawahamii mijini?
   A. Kubuni nafasi za kazi
   B. Kunadhifisha vijiji
   C. Kuwapa watu nafasi za kazi mashambani
   D. Kupeleka baadhi ya huduma mashambani

47. Neno ' amali' limetumika katika kifungu kumaanisha?
   A. Kazi    B. Ujira
   C. Ajira    D. Mali

48. Kulingana na aya ya mwisho, ni kawaida maishani
   A. Watu kufanana
   B. Kuwa na tofauti katika kazi zifanywazo
   C. Kutokuwa na rangi moja
   D. Watu kutochukia kazi nyingine

49. ' Mwelekeo wa watu kuhusu kazi za mikono lazima ubadilike? Kauli hii inamaanisha nini?
   A. Watu wanazichukia kazi za mikono
   B. Malipo ya kazi za mikono ni duni
   C. Wanaofanya kazi za mikono ni maskini
   D. Wasiozithamini kazi za mikono wabadilishe mawazo yao

50. Kichwa mwafaka kwa kifungu hiki ni:
   A. Kazi
   B. Kazi mbalimbali
   C. Kazi na ajizi
   D. Thamani ya kazi